

Kitambulisho cha Kipekee cha Mwanafunzi

Taarifa kwa wazazi na walezi

Serikali ya Australia inahitaji kila mtu anayechukua sifa za mafunzo zinazotambulika kitaifa kuwa na Kitambulisho cha Kipekee cha Mwanafunzi (USI).

Hii inajumuisha wanafunzi wa shule wanaojiandikisha katika sifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) kama sehemu ya programu yao ya shule.

USI ni nini?

USI ni namba ya elimu ya mtu binafsi ambayo hudumu kwa mtu maisha yote. USI huwezesha upatikanaji wa kumbukumbu za mafunzo na matokeo ya mtu katika akaunti ya mtandaoni anayodhibiti.

Inahitajika wakati wa kujiandikisha kwa ajili ya masomo zaidi na shirika lolote la mafunzo.

USI inapatikana bila malipo na itachukua kama dakika 5. Akaunti ya mtandaoni ya USI inaweza kupatikana mtandaoni wakati wowote.

Je, mwanafunzi anawezaje kuunda au kufungua USI?

1. Wanafunzi watahitaji aina mbili za vitambulisho kati ya zifuatazo kabla ya kuanza kutuma maombi:
 - Leseni ya Udereva
 - Kadi ya Medicare
 - Pasipoti ya Australia
 - Visa (iliyo na Pasipoti Isiyo ya Australia) kwa wanafunzi wa kimataifa
 - Cheti cha Kuzaliwa cha Australia, tafadhali kumbuka kuwa dondoo ya Cheti cha Kuzaliwa haitoshi
 - Cheti cha Usajili Kwa Nasaba
 - Cheti cha Uraia
 - ImmiCard

Kwa taarifa zaidi kuhusu fomu za kitambulisho nenda kwenye

<http://www.usi.gov.au/help-centre/proof-of-ID/Pages/proof-of-ID.aspx>

Maelezo yaliyowekwa lazima yalingane na maelezo yaliyoonyeshwa kwenye fomu ya kitambulisho kilichotumiwa. Kwa kutumia aina ya kitambulisho kilichoorodheshwa hapo juu USI inapoundwa, inaruhusu Serikali kumtambua mtu huyo ili kuhakikisha kwamba USI ni ya kipekee kwa mtu huyo.

2. Hakikisha kwamba maelezo binafsi ya mawasiliano ya mwanafunzi yameandaliwa, kama vile anwani ya barua pepe.
3. Nenda kwenye tovuti ya USI <https://www.usi.gov.au/students/get-a-usi>.
4. Bonyeza kwenye kitufe cha 'Bonyeza hapa ili Kupata USI yako' na ufuate hatua.

5. Ikiwa mwanafunzi anasomea sifa za VET, USI lazima itolewe kwenye shule ya mwanafunzi.

Unaweza kupata taarifa kuhusu USI katika lugha zingine kwenye <https://www.usi.gov.au/languages>.